



JESHI LA ULINZI LA WANANCHI WA TANZANIA

Simu ya Upepo "**N G O M E**"
Simu ya Mdomo: "**DOM + 255737962064**"
Telex: "**+255 (26) 2963757**"
Fax: "**+ 255 262 962153**"
Barua pepe: ulinzimagazine@tpdf.mil.tz
Tovuti: [www\(tpdf.mil.tz](http://www(tpdf.mil.tz)

Makao Makuu ya Jeshi,
Sanduku la Posta 194,
Dodoma, Tanzania
02 Februari, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limekuwa likishiriki shughuli za Ulinzi wa Amani chini ya Mwamvuli wa Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

JWTZ limeshiriki kulinda Amani katika nchi mbalimbali ikiwa ni pamoja na nchini Lebanon, Sudan, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Liberia, Msumbiji pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Aidha, katika ushiriki wetu, JWTZ linaendelea kulinda amani kwa Mwamvuli wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika huko Mashariki mwa nchi ya DRC (SAMDRC) eneo ambalo limekumbwa na mgogoro uliozua mashambulizi kati ya Waasi wa M23 wanaopambana na Jeshi la DRC (FARDC) katika maeneo hayo.

Kufuatia mashambulizi ya mfululizo katika maeneo ya SAKE na GOMA yaliyofanywa na Waasi wa M23 tarehe 24 na 28 Januari 2025, JWTZ limewapoteza Askari wake idadi wawili (02) na wengine idadi wanne (04) kujeruhiwa. Majeruhi wanaendelea kupatiwa matibabu mjini Goma.

Taratibu za kuisafirisha miili ya Marehemu wetu pamoja na majeruhi waliotokana na mapigano hayo zinaendelea kuitia Sekretarieti ya SADC. Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka majeruhi wetu na aziweke Roho za Marehemu Mahali Pema Peponi, Amina.

Aidha, vikundi vyetu vilivyopo nchini DRC viro salama, imara na vinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa maelekezo ya Uongozi wa SADC.

Imetolewa na



Kanali Gaudentius Gervas Ilonda

Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano

Jeshi la Utinzi la Wananchi wa Tanzania

